

# MOLA WANGU NI ALLAH

سواحلي

Kuishi pamoja  
na Allah na  
majina yake na  
sifa zake

www.with-allah.com



D. Muhammad bin sarrary Alyamaniy  
D. Abdullah ibn Saalim Bahamam

## Kuishi pamoja na Allah na majina yake na sifa zake:

### a-yeye ni Allah.

### Allah Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu

Yeye ni Allah Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

Ameandika rehema katika nafsi yake,na rehema zake imetangulia ghadhabu zake,na rehema zake zimeenea kila kitu.

{Bila shaka rehema ya Mwenyezi Mungu iko karibu sana na wanaofanya mema} (Al-a'araf : 56)

Hakika yeye ni Mwingi warehema Mwenye kurehemu'

Ana huruma kwetu zaidi kuliko huruma ya mamazetu kwetu, asema Mtume (s.a.w) kuashiria mwanamke anayemnyonyesha mwanawe.: ' Je! Mwamuona huyu anaweza kumtupa mwanawe motoni? Tukasema la1 haiwezikani,akasema Mtume(s.a.w) basi Allah anahuruma kwa waj awake kuliko huyu mama kwa mtoto wake.' Imepokewa na Albukhari

Hakika yeye ni Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

Anarehema viumbe vyote, na amewatengea waumini rehema makhsusi kwao , {Naye ni Mwenye kuwarehemu sana waislamu} (Ahzab : 43)

Hakika yeye ni Mwenye kurehemu'

Miongoni mwa rehema zake nikututumia Muhamad (s.a.w) kuwa rehema kwa walimwengu wote, awe

Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu,Mwema ,Mkariim, mwenye kujibu maombi ya waja wake, Mwenye huruma,Mwenye kutoa .haya majina maana yake yanakaribiana, na yote yaonesha kuwa Allah anasifika na rehema na wema na ukarimu ,yote yaonesha kuenea kwa rehema zake ambazo zimeenea kila kitu, kulingana na hekima yake,na akawajalia waumini kuwa na fungu kubwa, na sehemu kamilifu, amesema Allah Mtukufu: { Na rehema yangu inaweza kukienea kila kitu lakini nitawaandikia wale wanaojikinga na yale niliyowakataza,[A'araf :156] neema na wema zote hizi ni athari za rehema yake Allah na ukarimu wake na kheri za duniani na za akhera zote ni athari za rehema zake.



mwenye kuongoa watu wote, mwenye kuwahifadhi maslahi yake ya kidunia na yakiakhera.

Hakika yeye ni Mwenye kurehemu'

Hakuna mwenye kuzuia rehema zake isipokuwa yeye mwenyewe, na hakuna mwenye kuziachilia isipokuwa yeye mwenyewe. { Rehema anayoifungua Mwenyezi Mungu kwa watu, hakuna wa kuzuia; na anayoizua hakuna wa kuipeleka mbele (isipokuwa atakapotaka) naye ni Mwenye nguvu, Mwenye hikima.} (Fatir: 2)

Hakika yeye ni Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.

## **Mwenyezi Mungu Mwenye kutoa na Mwenye kukubali maombi ya waja wake.**

Hakika yeye ni Allah Mwenye kutoa na Mwenye kukubali maombi ya waja wake.

Ewe Mwenye kutoa neema Ee Mwenye kutoa matumaini Ewe Mwenye kutoa wema.

Naomba unipe mapenzi unipe matumaini unipe raha na huruma!

Tuonee huruma na utufadhili, kwasabab wewe ndiwe mwenye fadhila na huruma na mkarimu. {Na utupe rehema itokayo kwako; hakika wewe ndiwe Mpaji mkuu.} (Aali imran : 8) 'Hakika Allah ni Mkarimu anapenda ukarimu na tabia za hali ya juu, na hapendi tabia duni.' (Imepokewa na Atirmidhiyu)

**"MPAJI MKUU"**

Anampa amtakaye na humnyima amtakaye .

**"MWENYE KUTOA"**

Kutoa kwake hakuna mipaka, na fadhila zake hakuna wakuzizuia, akitaka kitu husema :

{Kuwa na kina kuwa} (Albaqarah :117)

**"MPAJI MKUU"**

Anatoa riziki inayoonekana na riziki isioonekana, na hutoa kwa fadhila zake na ukarimu wake.

Miongoni mwazo ni pale Allah anpomfungulia mja wake mawazo mazuri, na mawazo yaliyo na manufaa, na elimu na uongofu na tawfiq na kukubaliwa maombi yake, yote haya na mengineyo ni riziki isioonekana, aliyo wapa watu wengi.

**"MPAJI MKUU"**

Ametoa akazuia, akadhililisha na kuenua, ameunga na akakata, kwake ziko kheri zote hakika yeye ni Mweza wa kila kitu.

**Hakika yeye ni Allah Mpaji Mkuu Anayetoa bila mipaka.**

**Allah aliye na wasaa.**

Hakika yeye ni Allah aliye na wasaa {Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa (mkubwa sana) na Mwenye kujua (kukubwa vile vile)} (Albaqarah : 115)

**"Mwenye wasaa"**

Mtoaji atosheleza yote aombwayo

**"Mwenye wasaa"**


Aliye kamilika katika sifa zake, Mtukufu katika majina yake, hazihesabiki sifa zake njema, anawasaa wa utukufu na waufalme na wautawala na wafadhila na wakutoa na wawema.

**"Mwenye wasaa."**

Anawatosheleza viumbe wake wote kwa kuwapatia na kuwatosheleza na kuwaelimisha na



<https://www.with-allah.com/sw>



kuwajua na kuwahifadhi na kupanga mambo yao.

**"Mwenye wasaa"**

Ambaye yameenea masikio yako sauti zote wala hazimchanganyi lughaa.

**"Mwenye wasaa"**

Amewafanyia wepesi waja wake na akaifanya dini kuwa nyepesi na akawawezesha Allah Mwenye nguvu na utukufu.

**Hakika yeye ni Allah Mwenye wasaa.**

## **Allah Mwenye kupenda waja wake**

Hakika Allah ni Mwenye kupenda waja wake { Na yeye ni Mwingi wa msamaha Mpenda waja wake} (Al-baqarah : 14)

Allah Mwenye kupenda waja wake, anawapenda na kuwakaribisha na kuwaridhia nao wanamridhia. {Anawapenda nao wanampenda} (Almaidah:54)

Allah anawaruzuku mapenzi ya watu kwao, watu wanawapenda na kuwakubali walionayo.

**Mpenda waja wake'**

Aliye karibu Mwenye kupenda waja wake, Mwenye kuwapendea kheri waja wake

**Mpenda waja wake'**

**“Mpenda waja wake”, anayewapenda Mitume yake na Manabii wake, nawafuasi wao, na kuwapenda, kwahio nikipenzi kikubwa kwao kuliko chochote. Nyoyo zao zimejaa mapenzi yake, na ndimi zao zimezoea kumsifu yeye, na nyoyo zao zimejivuta kwake kwa kumpenda na kumtakasia yeye ibada na kurudi kwake kwa aina zote za kurudi.**

Waja wake wanampenda na wako na shauku ya kukutana naye, katika hadeeth:

‘Mwenye kutamani kukutana na Allah naye Allah hutamani kukutana naye.’  
(Imepokelewa na Albukhaar.)

**“Mpenda waja wake”**

Anakuamrisha kutakasia moyo wako, na kuusafisha kutokamana na chuki na bughdha, na kuoga uchafu wa chuki kwenye maji ya mapenzi nakupendana, na kuzima moto wa hasad kwa barafu (theluji) ya mapenzi na kupendana.

**Hakika yeye ni Mpenda waja wake**

## **Allah Mwenye uhai wa milele na Mwendeshaji wa mambo yote**

Hakika yeye ni Allah Mwenye uhai wa milele na Mwendeshaji wa mambo yote. {Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa yeye -

Mwenye uhai wa milele, na Mwendeshaji wa mambo yote.} (Aali Imran : 2)

Hakika yeye ni Allah Mwenye uhai wa milele. {Mwenyezi Mungu, hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa yeye - Mwenye uhai wa milele, na Mwendeshaji wa mambo yote.} (Aali Imran : 2)

**“Mwenye uhai wa milele”**

Uhai uliokamilika, haitajii yeyote, na wasiokuwa yeye wote wanamuhitaji yeye, na vyote vitaangamia na kwisha isipokuwa dhati yake Allah,

**Mwendeshaji wa mambo yote**

Mwenye kujitosheleza mwenyewe, haitajii yeyote

**Mwendeshaji wa mambo yote**

<https://www.with-allah.com/sw>

Msimamizi wa kila nafsi na iyatendayo, Mwenye kuhifadhi matendo yao na hali zao na mazungumzo yao, na mema yao, na maovu yao, atakayewalipa kwa matendo yao haya aakhera.

**Mwendeshaji wa mambo yote**

Mwenye kukusanya na kuyajua yote waliotenda waja wake.

**"Mwenye kupanga mambo yote"**

Aliyebeba dhamana ya maisha ya kila kiumbe chake, na riziki zao, na mwenendo wao, na hali zao, na kupangilia mambo yao.

**"Mwenye uhai wa milele na Mwendeshaji mambo yote"**

Mwenye ku bakia bila kuondoka ametakasika na kutukuka.

**Hakika yeye ndie Allah Mwenye uhai wa milele na Mwendeshaji mambo yote.**

## **Allah Anaye fanya analo litaka**

Hakika yeye ni Allah Mwenye utukufu wa hali ya juu, na Anayefanya alitakalo. {Yeye ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye tu. Mfalme, Mtakatifu, Mwenye salama, Mtoaji wa amani, Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo yake, Mwenye nguvu, Anaye fanya analo litaka, Mkubwa, Ametakasika Mwenyezi Mungu na hayo wanayo mshirikisha nayo.} (Alhashri: 23)

**"Anaye fanya analolitaka."**

Mwenye kumlazimasha mjeuri na Mwenye kumsaidia mateka, Mwenye kumtoshela fakiri, Mwenye kuunganisha pungufu za wenye upungufu, Mwenye kusamehe madhambi ya wenye kukosea, Na Mwenye kuwaacha uhuru waliotakiwa kuadhibiwa, Mwenye kuziunga nyoyo za wapendanao na wanyenyekevu.

**"Anaye fanya analolitaka"**

Ambaye umekamilika Ukubwa wake, na kutukuka neema zake kwa kila kitu.

**"Anaye fanya analolitaka"**

**Mwenye uhai na Mwendeshaji mambo yote**

**Uhai uliokamilika anayejisimamia mwenyewe, Mwenye kusimamia viumbe wa mbinguni na wa ardhini, Mwenye kupangia riziki zao na hali zao tafauti tafauti.**

**"Mwenye uhai wa milele"**

**Aliye kusanya sifa zote za dhati, Mwendeshaji mambo, Aliye kusanya sifa zake zote.**

Ambaye amekubaliwa na kila kitu, na kunyenyekea kwake kila kitu, wala hakuna kilicho mshughulisha kwa kutenda chochote.

**"Anayefanya analolitaka"**

Mwenye uwezo wa kufanya lolote, Mwenye ufalme na utawala na ukubwa na heshima zote.

**"Anaye fanya analolitaka"**

Wamedhalilika majabari wote, na kunyenyekea kwake wakubwa wote, na kudhalilika kwake wafalme wote na wakubwa wote, na kunyenyekea mbele yake waliofanya makosa (waovu).

**Hakika yeye ni Allah "Anayefanya analolitaka"**

## **Allahu ni Mzuri**

**Hakika yeye Allah ni Mzuri Mtukufu**

'Ewe Allah twakuomba ladha ya kukutizama dhati yako tukufu, na tu na shauku kweli ya kukutana nawe'

**"Mzuri"**

Yuko na majina yale yalio mazuri zaidi, na sifa zilizokamilika.

**"Mzuri"**

Uzuri wa majina uliokamilika na uzuri wa sifa zilizo kamilika na uzuri wa ukamilifu wa kikwelikweli.

**"Na yametimia maneno ya Mola Mlezi wako kwa kweli na uadilifu."**  
(Al-an'am : 115)

Ambaye ametengeneza vizuri umbo la kila kitu

**"Mzuri"**

Uzuri wa vilimwengu ni ushahidi tosha ya uzuri wake Allah na utukufu wake; uzuri wake Allah hauwezi kufikiwa na akili, wala hauwezi kujulikana uhakika wake kwa fahamu za watu.

Amesema Mtume (s.a.w) **'Siwezi kukusifu vilivyo Ewe Allah kama ulivyo jisifu mwenyewe.'** (Imepokewa na Muslim.)

**"Mzuri"**

Aliyetowa uzuri kwa viumbe na uzuri wao, na akatoa uzuri wa kumdhania

**"Anayefanya analolitaka"**  
kwa maana yeye yuko juu ya waliojuu wote, Mwenye nguvu, yani Mwenye huruma, Mwenye kuunga nyoyo zilizo vunjika, Mwenye kumsaidia mnyonge asiyejiweza, kila aliye mtegemea na kurudi kwake.







yeye kwamba ni Mzuri Asie na kifani.

Ewe Mzuri! Unayependa vizuri, twakuomba uzifanye nzuri nyoyo zetu kwa imani, na uzipe tabia zetu uzuri na nyoyo zetu uzuri, na dhahiri yetu uzuri.

**Hakika yeye ni Allah aliye Mzuri**

## **“Allah Mwenye kujua kila kitu Mwenye kujua yaliyo ya dhahiri Mwenye kukusanya”**

Hakika yeye ni Allah Mwenye kujua kila kitu, Mwenye kujua yaliyo ya dhahiri, na Mwenye kukusanya yote.

**“ Mwenye kujua kila kitu, Mwenye kujua yaliyo ya dhahiri Mwenye kukusanya”**

Ambaye elimu yake imeenea kila kinachoonekana na kilichofichika, cha siri na cha jahari, vinavyowezikana na visivyo wezikana, anayejua viumbe vyote vya juu na vya chini,

anayejua ya sasa na yaliopita na yatakayo kuja; hakifichiki chochote kwake.

Mwenye kujua kila kitu, Mwenye kujua yaliyodhahiri. {Hakika kuijua Saa (ya Kiyama) kuko kwa Mwenyezi Mungu. Na Yeye ndiye anaye iteremsha mvua. Na anavijua viliomo ndani ya matumbo ya uzazi. Na haijui nafsi yoyote itachuma nini kesho. Wala nafsi yoyote haijui itafia nchi gani. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kujua, Mwenye khabari.} (Luqman :34) {Allah Mwenye kujua kila kitu Mwenye kukusanya } {Anajua viliomo katika mbingu na ardhi, na anajua mnayo yaficha na mnayo yatangaza. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa yaliomo vifuani.} (At-taghabun :4)

Yeye ni Mjuzi wa kila kitu {Mwenyezi Mungu ni yule ambaye ameziumba mbingu saba, na ardhi kwa mfano wa hizo. Amri zake zinashuka baina yao, ili mjue kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu, na kwamba Mwenyezi Mungu amekizunguka kila kitu kukijua vilivyo kwa ilimu yake} (At talaq : 12)

Na amesema Allah Mtukufu: { Na kwamba Mwenyezi Mungu amekizunguka kila kitu kukijua vilivyo kwa ilimu yake} (At talaq : 12)

**Hakika yeye ni Allah Mwenye kujua kila kitu Mwenye kujua yaliyo ya dhahiri Mwenye kukusanya**

## Allah Aliye karibu

Yeye ni Allah aliye karibu

Ewe uliye karibu na anayekuomba, ewe uliye karibu na anaye kutaraji.

Ewe uliye karibu na anaye kuomba. eweulie karibu nasi kuliko mshipa wa shingo.

Twakuomba utupe utulivu wako na utuliwaze na maneno yako, {Na waja wangu wangu watakapokuuliza hakika yangu,Mimi niko karibu nao.} (Albaqarah : 186)

“Aliye karibu”

Yuko karibu nasi kwa elimu yake na vile anavyo tuona japokuwa yuko mbinguni.

“Aliye karibu”

Kwa mwenye kumuomba, anampa na anamuonea huruma, na anamwenua na kumuondolea madhara na kumuitikia aliye na matatizo.

“Aliye karibu”

Kwa mwenye kutubia kwake na kushikana naye, anasamehe dhambi na kukubali toba.

“Aliye karibu”

Anayakubali anayojikaribisha kwake mja wake nayo,na anamkaribia mja wake kwa kadri mja anavyo jikaribisha kwake.

“Aliye karibu”

Anayezijua hali za waja wake, kwasababu yeye yuko karibu nao kwa elimu yake na kuzunguka kwake, wala hakuna chochote kinachofichika kwake.

“Aliye karibu”

Karibu kwa upole wake na kuhifadhi kwake na kunusuru kwake na kuunga mkono kwake, lakini ukaribu huu ni maalumu kwa vipenzi vyake.

“Aliye karibu”

Wanarudi kwake waja wake baada ya kifo chao. “Nasi tunakaribiana naye zaidi kuliko nyinyi” (Al-waqiah : 85)

“Aliye karibu”

Nafsi zinaliwazika kwa kuwa karibu naye, na zinatingishika kwa kumtaja na kumkumbuka.

**“Aliye karibu” ukaribu wa kila mtu kwa elimu yake na ujuzi wake na kulindiza kwake na kuona kwake na kuzunguka kwake.**

Hakika yeye ni Allah Aliye karibu

## Allah Mwenye kupokea maombi ya waja wake

Yeye ni Allah Mwenye kupokea

“ Hakika Mola wangu ni karibu na waja wake anapokea maombi yao.” (Hud :61)

“Mwenye kupokea”

Anapokea maombi ya waja wake wakimuomba na kutawasili kwake kwa yale alio waamrisha, yeye ndie aliye waamrisha kumuomba, kisha akawaahidi kujibu maombi yao.

“Mwenye kupokea”

Ameshikana naye mfungwa gerezani, mfa-maji baharini, na fakiri katika ufakiri wake, na yatima katika uyatima wake, na mgonjwa katika ugonjwa wake, na tasa katika utasa wake, akampa na kupokea na kumsaidia na akaponya.

“Mwenye kupokea”

Anamjibu aliyedhikika {Au Yule anayemjibu aliyedhikika amwombapo na kuondoa dhiki yake.} (An-namli :62)

“Mwenye kupokea” anamjibu anaye muomba hata haweje, hata hawe wapi, na hata wawe hali gani.

Na anakuwa zaidi ya kujibu anapombwa kwa kutawasali kwake kwa majina yake na sifa zake, kwani wangapi walimuomba wakiwa gerezani naye akawatoa, na wangapi waliotawasali wakiwa baharini na akawaokoa, na wangapi waliomba riziki wakiwa mafakiri naye akawafanya matajiri na kuwapa amani, na mayatima wangapi walimuomba naye akawalea na kuwachunga mpaka wakawa wakubwa, na ni wagonjwa wangapi walimtaraji naye akawaponya na kuwafanya wawe salama, na wangapi walikuwa tasa wakanyenyekea kwake naye akawaruzuku watoto na akawakirimu.

Hakika yeye ni Allah Mwenye kupokea

## Allah ni Nuru

Hakika yeye ni Allah Nuru

{Mwenyezi Mungu ni Nuru ya Mbingu na Ardhi.} An-nur : 35

“ NURU ”

Aliyemwilika nuru yake kwenye nyoyo za wenyekumjua kwa maarifa yake na imani, na akamwilika vifua vyao kwa mwongozo wake.

“Nuru”

Aliondoa giza kwa nuru yake na akamwilika mbingu na ardhi , na kamwilika njia kwa wenye kuifuata nyoyo zao

Allah ni Nuru na sitara yake ni nuru ,kama ataifunua tu vingeingua kila kitu ambacho kinaelekea nuru hio.

**Hakika yeye ni Allah Nuru**

## **Allah Mwenye Hekima**

Hakika yeye ni Allah Mwenye hekima {Kwani Mwenyezi Mungu si muadilifu kuliko mahakimu wote?}(At-tin :8)

**“ Mwenye hekima”**

Ambaye anahukumu vitu na kuvieka kwenye hali nzuri, na anavieka sehemu yake ambayo inafaa kwa kudura zake Allah Mtukufu.

**“ Mwenye hekima”**

Alieka sharia kwa hekima yake, na akaeka suna kwa hekima yake, sharia zake ni hekima tupu katika makengo yake na siri zake na mwisho wake wakidunia na wakiakhera.

**“ Mwenye hekima”**

Mwenye hekima katika alivyopanga na kuamua, Mwenye hekima katika kumjalia fakiri kuwa fakiri, na kumfanya mgonjwa abaki na ugonjwa wake na unyonge wake, na kumfanya mdaiwa kubaki katika dhiki yake na kutopata chakulipa deni lake, hakuna dosari yoyote katika mipango yake, wala maneno yake na vitendo vyake haviingii dosari yoyote, yuko na hekima ya hali ya juu.

**“ Mwenye hekima”**

Anaye wapatia ilhamu waja wake ya hekima na maarifana wekevu na upole na kuweka mambo katika sehemu yake sahihi.

Allah ni muadilifu kuliko mahakimu wote, hakutokei kitu chochote ulimwenguni isipokuwa kwa idhini yake, yeye pekee ndie anahalalisha na kuharamisha, hukumu ni ile aliohukumu yeye, na dini ni ile alio amrisha au aliokataza, hakuna mwenye kumuuliza kwasababu gani kahukumu hivyo, na hakuna wakupinga amri na kadari yake.

**“Mwenye hekima” yeye Ndie aliye na hekima za hali ya juu katika kuumba kwake na kuamrisha kwake, hajjumbii kitu hovyoya bila sababu, wala haamrishi jambo bila sababu, Ambaye hukumu ni yake Yeye mwanzo na mwisho.**

“ Mwenye hekima”

Hamdhulumu yeyote ... Muadilifu katika amri zake na makatazo yake na habari zake.

Hakika yeye ni Allah Mwenye hekima Mwenye kuhukumu.

## Allah ni Mfalme Mwenye kumiliki.

Hakika yeye ni Allah Mwenye kumiliki

{Mfalme, Mtakatifu}

(Al-hashri : 23)

“Mfalme”

Mwenye ukubwa na utawala anapanga mambo ya waja wake na anafanya atakavyo, kwani wao ni waja wake na wanamuhitaji yeye, Naye ni Mfalme wao na Mwenye Kuwamiliki.

Anao utawala wa hakika, kwasababu hakuna Mfalme wala Raisi isipokuwa naye ni mmilikiwa na yeye, hakuna heri yoyote duniani wala akhera isipokuwa inatoka kwake na ni fadhila zake. {Ni vyake pekee vyote viliomo mbinguni na duniani.} (Al-baqarah : 255)

“Mfalme”

Anatoa bila hesabu, na anawapatia kwa kumwaga waja wake, wala hakipungui chochote katika milki yake, wala halimshughulishi jambo lolote akaacha lengine. Katika hadiith qudsi sahihi amesema Allah: Lau wamwanzo wenu na wa mwisho wenu, na wanadamu wote na majini wote watasimama katika uwanja mmoja na wote waniombe na nimpe kila aliyeomba alichokiomba haipunguzi lolote katika hazina yangu, bali ni mfano wa kuingiza sindano kwenye bahari na itoke na toni, (Imepokewa na Muslim)

“Mfalme Mwenye kumiliki”  
Ambaye ana ufalme, anasifika kwa sifa ya kumiliki, nayo ni sifa ya ukubwa na utukufu na nguvu na kupanga, Ambaye ndiye mfanyaji wa vitu kwa hakika bila mipaka, katika kuumba na kuamrisha na kulipa, na ulimwengu wote wa chini na wajuu ni wake yeye, wote ni waja wake na wenye kumilikiwa naye, na wenye kumuhitaji yeye.

### “Mfalme”

Humpa ufalme wake amtakaye. Amesema Allah Mtukufu: {Sema: Ewe Mwenyezi Mungu uliye miliki ufalme wote! Wewe humpa ufalme umtakaye, na humwondolea ufalme umtakaye, na humtukuza umtakaye, na humuangusha umtakaye. Kheri yote iko mikononi mwako. Hakika Wewe ni Muweza wa kila kitu} [aali'imran : 26]

### “Mfalme”

Mwenye kuwamiliki waja wake anayeendesha mambo yao ya dunia na akhera; basi yeye yapaswa apendwe na ukusudiwe, na watu waongeze tamaa ya kuyaomba yaliyo kwake, kwa kuomba na kutaka na kulalamikia na kumuita yeye Allah pekee.


**Hakika yeye ni Allah Mwenye hekima Mwenye kuhukumu**

## Allah Mtukufu

### Hakika yeye ni Allah Mtukufu

Ametukuka katika utukufu wake, na ametakasika kwenye sifa zake. {Yeye ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye tu. Mfalme, Mtakatifu, Mwenye salama,} (Al-hashri : 23)

Ametukuka na kutakasika Mola wa Malaika na Roho Mtakatifu (Jibril) Ametukuka Mfalme Mtukufu.



**, “Mtakatifu, Mwenye salama” Mwenye kutukuzwa na kutakaswa kutokana na sifa zote za upungufu, yeye ametakasika na aibu zote na ametakasika hakuna anaye mkaribia wala kufanana naye katika kitu chochote katika ukamilifu wake,**

### “Hakika yeye ni Allah Mtukufu”

Mwenye kutukuzwa na kutakaswa na kila aibu na pungufu, na kutokana na sifa yoyote ambayo hailingani naye Mtukufu .

### “Hakika yeye ni Mtukufu”

Anayesifika na sifa kamilifu, nzuri na tukufu, Mwenye kutakaswa kutokana na pungufu na aibu, Hapana kitu kama mfano wake, Wala hana anaye fanana naye hata mmoja, hakuna ukamilifu juu ya ukamilifu wake, wala hakuna anayemfikia kwa majina yake na sifa zake.

### “Hakika yeye ni Mtukufu”

Ambaye ametukuzwa na nyoyo zote, na kufungana naye kila matamano yake, ametukuzwa na ndimi, akatukuzwa katika kila wakati.

### “Hakika yeye ni Mtukufu”

Mwenye Baraka na zawadi, na fadhila na sifa nzuri, Baraka yatoka kwake na kurudi kwake, naye Mwenyewe ni Baraka anaye bariki waja wake kwa atakacho katika kuwapa na kuwaongezea.

### “Hakika yeye ni Allah Mtukufu”



## Allah ni Amani(Mwenye salama)

**“Hakika yeye Allah ni Amani”**

Allah ni Mwenye salama (amani) na kwake yatoka salama, hapati mja amani na salama isipokuwa amani na salama kutoka kwake, na kufaulu hakukamiliki isipokuwa kwa tawfiq yake Mtukufu.

**Hakika yeye ni Mwenye salama,”**

Aliye salimika na kila pungufu na aibu, Mwenye kuwasalimisha wengine kutokana na matatizo na shari.

**Hakika yeye ni Mwenye salama,”**

Sifa zake zimesalimika na kufananishwa na viumbe pia kuekwa sawa navyo, Amesalimika kutokana na pungufu zote, na sifa zake zote zimesalimika kutokamana na sifa zote pungufu, elimu yake imekamilika tena ikasalimika, uadilifu wake ni kwakila kitu na uliosalimika, ufalme wake umekamilika na umesalimika na hukumu yake pia imesalimika, kadhaa yake pia imesalimika, yeye

ni salamu na kwake yatoka salamu ametakasika Mola Mwenye cheo na Ukarimu.

Allah amejalia waja wake salama katika nyumba mbili( dunia na akhera) **“{Iwe salama kwa Ibrahim!} (As-swafat) {Iwe salama kwa Musa na Haruni!} (As-swafat 120) {Na Salamu juu ya Mitume} (As-swafat: 181)**

Na akhera amesema Allah Mtukufu: **{{(Watambiwa:) Ingieni kwa salama na amani}. (Al-hifr :46)**

**Mwenye salama,”**

Salama na amani iliyokamilika isiyokuwa na hofu baadaye, na msamaha usiyokuwa na uoga baadaye.

Yeye ni salama na kwake yatoka salama

**Mwenye salama,”**

## Allah ni Haki

Hakika Allah ni Haki {Hayo ni kwa sababu hakika Mwenyezi Mungu ndiye Haki,} (Al-hajj :6)

**"Allah ni Haki"**

Ni haki katika dhati yake na sifa zake, yeye amekamilika kwa sifa zake, kuwepo kwake ni kulazimiana na dhati yake, hakuna kitu kinaweza kuwepo isipokuwa atake yeye, yeye ndiye alikuwepo na ataendelea kuwepo na kusifika na utukufu wake na uzuri wake na ukaamilifu wake, na ataendelea kujulikana na kila zuri.

**"Allah ni Haki"**

Kauli yake ni haki, vitendo vyake ni haki, kukutana naye ni haki, Mitume wake ni haki, vitabu vyake ni haki, dini yake ni haki, kumwabudu yeye pekee bila kumshirikisha na chochote ni haki, na kila kitu kinaegemezwa kwake ni haki. {Hayo ni kwa kuwa Mwenyezi Mungu ndiye Wa Kweli, na kwamba wale wanao waomba badala yake, ni baat'ili, na hakika Mwenyezi Mungu ndiye Aliye Juu na ndiye Mkubwa.} (Al-hajj : 62)

**Hakika yeye ni Allah wa Haki**

## Allah ni Mtoaji wa amani, Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo yake,

Hakika Allah ni Mtoaji wa amani, Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo yake,{Yeye ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hapana mungu isipo kuwa Yeye tu. Mfalme, Mtakatifu, Mwenye salama, Mtoaji wa amani, Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo yake,} (Al-ha'shri :23)

**"Mtoaji wa amani"**

Anaye eneza amani baina ya waja wake, na utulivu baina ya viumbe, na utulivu katika wahyi wake. { Na anawalinda na khofu. } (Qureish :4)

**"Mtoaji wa amani"**

Muaminifu Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo yake Anayeshuhudia yanayo fanyika kwao .

**"Mtoaji wa amani"**

Hapunguzi thawabu za waja wake, wala hawaongezei adhabu, naye ni Mbora



wa fadhila na Mbora wakufadhilisha, na Mbora wa wema na kuneemesha.

**“Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo yake”**

Ametawala waja wake, na akawa juu yao kwa kuwaamrisha na akawamiliki, na akawachunga na kuona katika vitendo wavifanyavyo na hali zao, kwasababu yeye amewazunguka, kila jambo kwake ni jepesi, na kila kitu chamuitaji yeye. { Hapana kitu kama mfano wake. Naye ni Mwenye kusikia Mwenye kuona} (As-shuraa : 11)

Hakika Allah ni Mtoaji wa amani, Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo yake,

**“Mtoaji wa amani”**

Aliye jisifu Mwenyewe kwa sifa za ukamilifu, na kwa ukamilifu wa utukufu na uzuri, Yeye Ndiye aliyetuma Mitume, nakuteremsha vitabu vyake, kwa hoja na aya zilizo wazi, na akawasadikisha Mitume wake kwa miujiza na hoja zinazo oneshwa ukweli waliyokuja nayo.

**“Mwenye kuyaendesha Mwenyewe mambo yake”**

Mwenyekuona mambo yaliyofichika, na yaliyozikwa vifuani, Ambaye amekizunguka kila kitu kukijua.

## **Allah Mwenye msamaha Mwingi wa kusamehe anaye samehe sana.**

Hakika Allah ni Mwenye msamaha Mwingi wa kusamehe { Hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu Mwenye maghfira.} (Al-hajj : 60)

“Allah ni Msamehevu Mwingi wa maghfira Mwenye kusamehe”

Ambaye bado ajulikana kwa msamaha wake, nabado anasifika na sifa ya kughufiria na kusamehe waja wake, kila mtu anahitaji msamaha wake na maghfira yake, kama anavyohitajia rehema zake na ukarimu wake.

Ewe Uliyeahidi msamaha na maghfira kwa mwenye kufanya sababu zote. Amesema Allah Mtukufu: {Na hakika Mimi ni Mwingi wa Kusamehe kwa anaye tubia, na akaamini, na akatenda mema, tena akaongoka} (Taha : 82)

Twakuomba ewe msamehevu! Uturuzuku toba ya kikweli kweli, twajivua kabisa kutoka kwenye dhambi na kuyaacha kabisa, na twajuta kwa yale tuliyoyatenda ya makosa na madhambi, na twaazimia kutoyarudia tena na kushikamana na twaa yako twaomba utusamehe ewe Msamehevu.

Ewe Allah hakika wewe ni Msamehevu unapenda kusamehe, basi twaomba utusamehe, ewe Allah ulitwambia wewe ni msamehevu. {Waambie waja wangu ya kwamba Mimi ndiye Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.} (Alhijr : 49)

Tuhurumie na tusamehe Ewe Mwenye maghfira

Hakika Allah ni Mwenye msamaha Mwingi wa kusamehe

## Allah Mwenye kupokea toba.

Hakika Allah ni Mwenye kupokea toba. {Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu.} (At-tawba : 118)

**"Mwenye kupokea toba"**

Aliye amrisha toba kwa waja wake, kwake ni neema na ukarimu wake, bali aliwaahidi mengi zaidi ya hayo, nao ni kuyafanya mabaya kuwa mema.

**"Mwenye kupokea toba"**

Ambaye anawathibitisha waja wake katika toba, nakuwasaidia katika maamrisho.

**"Mwenye kupokea toba"**

Ambaye anawafiki waja wake kufanya toba, na anawahimiza katika hilo, na anawafanya kumpenda kwa kupitia hilo.

**"Mwenye kupokea toba"**


Ambayo anaikubali kutoka kwa waja wake, na anawathibitisha kwa hayo, na anyanyua daraja na anawafutia madhambi.

Allah Aliyetukuka na utukufu wake.

Hakika Allah ni "Mwenye kupokea toba"

**"Mwenye kupokea toba"**

Ambaye bado anakubali toba ya wenye kutubia, na anasamehe madhambi ya wenye kukosea, kila mwenye kutubia kwa Allah toba ya kweli Allah anakubali toba yake, yeye ni Mwenye kupokea toba kwa wenye kutubia mwanzo kwa kuwafikia kufanya toba na kuwakubalia, naye ni Mwenye kupokea toba baada ya kutubia kwao kwa kuwasamehe madhambi yao.



## Allah Mmoja wa Pekee.

**Hakika yeye ni Allah Mmoja Wa Pekee**

Ewe uliye peke yako katika dhati Yako, na peke yako katika Majina yako, na peke yako katika Sifa zako.

Twakuomba Ikhlas na mapenzi na bidii, Ewe Mmoja wa kipekee Ewe Mwenye kukusudiwa kwa haja zote.

**“Wa pekee”**

Katika dhati yake na majina yake na sifa zake, hana msaidizi wala anayefanana naye, wala aliye sawa naye wala anaye mkaribia. {Je, mnamjua mwenye jina kama lake?} (Maryam : 65)

**“Wa pekee”**

Wa pekee katika Uungu wake Anayesitahiki kuabudiwa, hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Allah, wala haifai kufanyiwa ibada yeyote ndogo au kubwa ila Allah Mtukufu.

**“Wa pekee”**

Mmoja Mwenye kukusudiwa, Mola Mwabudiwa, Nyoyo zimesadikisha, na macho yameshikamana na Mjuaji wa siri (Allah)

**“Mmoja Wa pekee”**

Allah aliwaumba waja kwa misingi ya kumpwekesha yeye pekee asiye kuwa na mshirika, hakuna aliyelekea mwengine asiye kuwa Allah kisha akafaulu, wala hakuna aliyeabudu asiye kuwa Allah kisha akapata raha, wala hakuna aliyemshirikisha na chochote kisha akafaulu.

**Hakika yeye ni Allah Mmoja Wa pee.**

**“Mmoja Wa pekee”**

**Aliye pekee kwa ukamilifu wote; hakuna mwenye kushirikiana katika hilo yeyote, na nilazima kwa waja kumpwekesha kwa akili na maneno na vitendo, kwamba wakubali ukamilifu wake usiokuwa na mipaka, na kuwa pekee katika aina zote za ibada .**

## Mwenyezi Mungu Mkusudiwa.

Hakika yeye ni Mwenyezi Mungu Mkusudiwa. {Sema: Yeye Mwenyezi Mungu ni wa pekee. Mwenyezi Mungu Mkusudiwa.} (Al-ikhlas : 1-2)

“Mkusudiwa”

Aliye kamilika katika Majina Yake na Sifa zake, haumtokei upungufu wala kasoro.

“Mkusudiwa”

Mkwasi (Tajiri) Aliyejitosheleza hahiitajii yeyote katika waja wake, na waja wote wanamuhitajia yeye. {naye ndiye anaye lisha wala halishwi} (Al-anam : 14)

“Mkusudiwa”

Mola Mwenye kupanga vitu na Mfalme Mwenye kuendesha mambo.

“Mkusudiwa”

Nyoyo zimemuelekea yeye katika haja zao naye akazipatia kila zilizo omba bila kuzinyima, na zikamuomba katika haja zao akazifariji na kuziondolea matatizo zao. Na kukubali maombi dua zao. Walimuomba waliomkata akawaunga, na walimuelekea wenye hofu akawapa amani, na walimtaraji wenye kumpwekesha akawafikisha, walimuomba wenye matatizo akawaondolea, na walishikamana naye waja wake akawainua daraja Allah Aliyetukuka.

Hakika yeye ni Allah Mkusudiwa.

“Mkusudiwa”

Anayekusudiwa na viumbe wake wote katika haja zao zote na mambo yao yakidharura, kwa ukamilifu wake katika dhati yake na majina yake na sifa zake na vitendo vyake.

## Allah Mwenye nguvu

Hakika yeye ni Allah Mwenye nguvu na utukufu.

{Na Mwenyezi Mungu ni Mtukufu Mwenye nguvu Mwenye hikima.} (Al-anfal 67)

Allah Mwenye nguvu Mwenye kushinda.

Ambaye hazimdhuru nguvu za mwenye nguvu yeyote, wala hashindwi na uwezo wa mwenye uwezo yeyote, ametakasika Allah Aliyejuu Anayeyajua mambo ya dhahiri.

**"Mwenye nguvu"**

Nguvu zake zimekamiliika na vikadhalilika viumbe vyote kwake, kila mwenye nguvu akawa dhaifu mbele yake, kila asiye kuwa yeye ni dhaifu, na kila kiumbe kwake ni dhaifu.

**"Mwenye nguvu"**

Anampa nguvu amtakae, na anamuondoshea nguvu amtakae, na humuangusha umtakaye. Kheri yote iko mikononi mwake. Amesema Allah aliyetukuka: {Hakika utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu.} (Yunus : 65)

Hakuna utukufu kwasababu ya nasaba wala ukoo wala mali wala sababu yoyote isipokuwa kutoka kwake (Allah)

**"Mwenye nguvu"**


Wala hawi mtu yeyote mtukufu isipokuwa atakayemfanya mtukufu, na wala mtu hawi na nguvu isipokuwa kwa fadhila zake, basi mtu kama anashikamana basi ashikamane na Allah, na mwenye kutaka utukufu basi aelekeze moyo wake kwa Allah. {Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye utukufu - Yeye, na Mtume wake, na Waumini} (Al-munafiqun: 8)

Hakika yeye ni Allah Mwenye nguvu.



**"Mwenye nguvu"**

**Mwenye nguvu zote: nguvu za kushinda, na nguvu za kukataa, na akakataa kuwa viumbe wanamfikia, kwasababu ukhalifa wote na utukufu ni wake.**



## Ee! Allah Mwenye nguvu Mwenye kushinda



Hakika yeye ni Allah Mwenye nguvu Mwenye kushinda Mwenye nguvu juu ya wanadamu na majini {Naye ndiye Mwenye nguvu juu ya waja wake, na ndiye Mwenye hikima na Mwenye khabari zote} (Alana'm : 18)

**"Mwenye nguvu juu ya waja wake,"**

Ameshinda waja wake kwa kuwa juu kwake na elimu yake na kuwazunguka na kuwapangia mambo yao na kwa kuwatambua kwasababu ya kuwa juu kwake, hakufanyiki kitu chochote katika dunia hii isipokuwa kwa idhini yake na elimu yake.

**"Mwenye nguvu juu ya waja wake,"**

Ameshinda wenye inadi na viburi kwa hoja zake kubwa kubwa, na kuwawekea wazi hoja za kuwa yeye pekee ndie anapaswa kuabudiwa kwasababu yeye ndie Bwana wa viumbe wote na yeye pekee ndiye mwenye majina mazuri mazuri na sifa za juu.

**"Mwenye nguvu juu ya waja wake,"**

Ameshinda madhalimu na waliopindukia mipaka kwa kiburi atawafufua siku ya kiyama wakiwa wanyonge. {Nao watahudhuria mbele ya Mwenyezi Mungu Mmoja, Mwenye nguvu.} (Ibrahim: 48)

**"Mwenye nguvu juu ya waja wake,"**

Anayotaka yeye Allah ndiyo yawa hakuna awezaye kuyazuiya katika waja wake, hata kama atakuwa mkubwa kiwango gani, kuumba kwake madhubuti, kunawashinda walio na nguvu, hata kama watafika wapi na nguvu zao. ukianza kusifu uzuri wake maneno huisha kuleta mfano wake hata kama utakuwa mfasaha kupindukia.

Hakika yeye ni Allah Mwenye nguvu Mwenye kudhalilisha na kushinda.

**"Mwenye nguvu juu ya waja wake,"**

**Mwenye kudhalilisha kila kitu ambacho kimetukuzwa na viumbe, na vikadhalilika kwake viumbe vyote kwasababu ya nguvu zake na uwezo wake uliokamilika.**

## Allah Mwenye kuruzuku

**Hakika Allah ni Mwenye kuruzuku**

{Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kuruzuku, Mwenye nguvu, Madhubuti.} (Adh-dhariyat : 58)

**"Mwenye kuruzuku"**

Ambaye kwake ndio kuna riziki za waja na vyakula vyao, naye Allah Mtukufu Humkunjulia riziki amtakaye, na humpimia amtakaye, ambaye kwake pekee ndio kunapangwa mambo, na Yeye ndiye Mwenye funguo za mbingu na ardhi. Amesema Allah Mtukufu {NA HAKUNA mnyama yoyote katika ardhi ila riziki yake iko kwa Mwenyezi Mungu. Naye anajua makao yake na mapitio yake.} (Hud : 6)

Amesema Allah Mtukufu: {Na wanyama wangapi hawawezi kujimilikia riziki zao! Mwenyezi Mungu anawaruzuku hao na nyinyi pia. Na Yeye ndiye Mwenye kusikia Mwenye kujua.} (Ankabut :60)

Amesema Allah Mtukufu: {Hakika Mola wako Mlezi humkunjulia riziki amtakaye, na humpimia amtakaye. Hakika Yeye kwa waja wake ni Mwenye kuwajua na kuwaona.} (Al-israi : 30)

Na amesema Allah Mtukufu {Na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila ya hisabu.} (Albaqarah : 212)


**" Mwenye kuruzuku"**

Kila mtu ni muhitaji kwake, na kwa riziki yake, anawaruzuku watu wote wema kwa waovu wa mwanzo mpaka wa mwisho.

**“ Mwenye kuruzuku”**

A n a m r u z u k u aliemkubali kwa moyo safi riziki iliyo kamili, na anamlisha aliye muomba kwa elimu na imani , na anamsaidia mtu kupata riziki ya halali anayesaidia katika kutengea kwa moyo, na kutengea kwa dini kwa mwenye kutaka.

**Hakika Allah ni Mwenye kuruzuku**



## Allah Mpole

**Hakika Allah ni Mpole**

{Hakika Mola wangu Mlezi ni Mpole kwa alitakalo.} (Yusuf : 100)

**Mpole**

Ambaye amewafanya viumbe kuwa wapole kwa wenzao na upendo na kusikitiana.

**Mpole**

Mwenye kutoa wema mwingi na zawadi kubwa kubwa.

**Mpole**

Mpole kwa waja wake {Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa waja wake} (Ash-shuraa : 19)

Anawapa yaliyokuwa ya kheri kwao katika dunia yao au akhera yao, na anawanyima na kuwazuia yaliyo mabaya kwao katika dini yao na dunia yao.

**Mpole**



Macho hayamfikilii bali Yeye anayafikilia macho. {Macho hayamfikilii bali Yeye anayafikilia macho. Naye ni Mjuzi, Mwenye khabari.} (Al-an'am : 103)

**"Mpole"**

Anajua yaliyo fichika , na anahesabu vitendo vidogo,hakifichiki kwake chochote usiku wala mchana, anayajua maslahi ya waja wake madogo kwa makubwa na anawafanyia upole.

**"Mpole"**

Ni Mpole kwa waja wake anapohukumu katika jambo Fulani, na anawasaidia akikadiria jambo, na anawafungulia milango ya faraja mambo yakijifunga na yakiwa magumu, na anawafanyia wepesi mambo yakiwa magumu ametakasika Allah.

**Hakika yeye ni Allah Mpole**

## **Allah Hakimu**

**Hakika Allah ni Hakimu**

{ Na Yeye ndiye Hakimu Mwenye kujua.} (Sabai : 26)

**"Hakimu"**

Anatufungulia katika rehema zake. {Rehema ambayo Mwenyezi Mungu anawafungulia watu hapana wa kuizuia. Na anayoizuia hapana wa kuipeleka isipokuwa Yeye.} (Al-faatih :2)

**"Hakimu"**

Allah atufungulie sisi na nyinyi katika baraka zake, na atupe katika fadhila zake na zawadi zake, na atuongeze katika msamaha wake.

Yeye ni Allah Hakimu Mwenye kufungua nyoyo zilizofungika, kwa funguo za uongofu na imani.

**"Hakimu"**

Anafungua milango ya rehema na kuwachotea, na kuwafunika na neema zake na kuzidisha, anawafungulia nuru za elimu na hekima kwenye akili zao na kuzipamba, na anafungulia nyoyo imani ili zipate kuongoka.

**"Hakimu"**

Ambae anaondoa matatizo kwa waja wake, na kuwafariji katika kila hami, na kuwaondolea kila shida, na kuwaondolea kila madhara.

**"Mpole"**

**Ambaye elimu yake imeenea vitu vyote, vya siri na vilivyojificha, na akajua yaliyo fichika ndani ya vitu vidogo, Mpole kwa waja wake waislamu. Anaye wafikishia maslahi ya upole wake na wema wake kwa njia wasizotarajia.**

### "Hakimu"

Ambaye anahukumu baina waja wake kwa hukumu zake za kisheria, na hukumu zake za kadari, na hukumu zake za malipo, aliyefungua macho ya wenye kusubiri, na akafungua nyoyo zao ili wamtambue, na mapenzi yake na kutubia kwake, na akawafungulia waja wake rehema na riziki tofauti tofauti.

### "Hakimu"

Atakayehukumu baina ya waja wake akhera kwa waadilifu

Hakika Allah ni Hakimu.

## Allah Anayetajirisha

Hakika Allah ni Tajiri Anayetajirisha

### "Tajiri"

Tajiri kwa dhati yake, aliye na utajiri uliokamilika, sifa zake na ukamilifu wake hauingii upungufu kwa njia yoyote, na hawi ila tajiri kwasababu utajiri ni sifa yake inayomlazimu, kama ambavyo daima ni Muumba na Muweza Mwema, haitajii yeyote Yule,

yeye ni Tajiri ambaye hazina za mbingu na ardhi ziko mikononi mwake, na hazina za dunia na akhera ziko kwake. Anayetajirisha waja wake wote utajiri.

### "Tajiri"

Ametosheka haitajii chochote kutoka kwa waja wake, haitaji kwao chakula wala kinywaji, hajawaumba ili apate wingi wa viumbe, au kupanga nguvu kutokana na udhaifu aliokuwa nao, au kutaka liwaza kwasababu ya upweke wake, bali wao ndio wanamuhitaji yeye chakula chao na kinywaji chao na mambo yao yote, amesema Allah Mtukufu: {Nami sikuwaumba majini na watu ila waniabudu Mimi. Na sitaki kwao riziki, wala sitaki wanilishe.} (Adhariat : 56-57)

### "Mwenye kutajirisha"

Anawatajirisha watu kutokana na ufakiri wao na haja zao, haipungui hazna yake kwa kutoa, waja wake hawahitajii mwengine asiye kuwa yeye, ametukuka Allah . kama ilivyokuja kwenye hadiith qudsi: Kama wamwanzo wenu na wamwisho wenu, wanadamu na majini watakuwa katika uwanja mmoja na waniombe

mimi na nimpe kila mtu alichokiomba haipunguzi chochote katika hazina yangu ila kama kuingiza sindano kwenye bahari na kuitoa.

(Imepokewa na Muslim)

**“Mwenye kutajirisha”**

Anawatajirisha baadhi ya waja wake kwa uongofu na kutengea nyoyo zao, kwa kumjua yeye na kumtukua na kumtakasa na kumpenda, anawatajirisha kwa mambo ambayo ni bora na kamilifu kuliko maslahi ya kidunia.

Ewe ambaye hazina yako haipungui kwa wingi wakutoa.. twaomba ututajirisha kwa ya halali na utuepushe nay a haramu; kwasababu Wewe ni Tajiri Mwenye kutajirisha.

**Hakika Allah ni Tajiri Mwenye kutajirisha**

## **Allah Mwenye uwezo**

Hakika Allah ni Mwenye uwezo. {Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza na ujuzi juu ya kila kitu.}(An-nisaa : 85)

**“Mwenye uweza na ujuzi”**

Ambaye amefikisha chakula kwa viumbe wote, na kawaumbia vitu ambavyo ni sababu ya maisha yao, akawapa na akavifanya ndivyo vinavyo muondoshea mwenye kiu kiu chake na mwenye njaa njaa yake, na kuyafanya maisha yake kuwa ya furaha.

**“Mwenye uwezo na ujuzi”**

Anayelisha nyoyo kwa aina nyingi za maarifa na elimu; ndio roho zipate kuishi na nafsi kupata ukunjufu.

Ewe Allah unayetokeleza mambo ya waja wako, na kuyapanga maisha yao duniani na akhera, twakuomba utuhifadhi, utusamehe na utuponye. {Na hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza na ujuzi juu ya kila kitu.} (An-nisaa : 85)

**Hakika yeye ni Allah Mwenye uwezo na ujuzi**

**“Mwenye uwezo”**  
Aliyefikishia kila  
kiumbe chakula,na  
akawafikishia viumbe  
wake riziki, na  
kuigawanya atakavyo  
kulingana na hekima  
yake na sifa zake.



## Allah Anatosha na Mwenye kutosheleza.

Hakika Allah Anatosha na Mwenye kutosheleza

Allah anawatosha waja wake, na anawatosheleza katika kila kitu. { Je! Mwenyezi Mungu si wa kumtosheleza mja wake?} (Az-zumar : 36)

Allah anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa, aliyasema maneno haya kipenzi chake Allah Ibrahim (a.s) alipotupwa kwenye moto; moto ukawa baridi tena yenye amani, na wakayasema masahaba wa Mtume (s.a.w) katika maneno yake Allah Mtukufu: {Kuna watu wamekukusanyikieni, waogopeni! Hayo yakawazidishia Imani, wakasema;} (Ali-imran : 173)

Wakasema { Mwenyezi Mungu anatutosha, naye ni mbora wa kutegemewa.. Basi wakarudi na neema na fadhila za Mwenyezi Mungu. Hapana baya lilio wagusa, na wakafuata yanayo mrithi Mwenyezi Mungu.} (Aali-imran : 173-174)

### “Muhasibu”

Anayewajua waja wake anayewatosheleza wanaomtegemea, mwenye kulipa waja wake kheri na shari, kulingana na hekima yake na kujua kwake vitendo vyao vidogo na vikubwa.

Allah ni Mzuri wa kuhisabu waja wake, Mwenye kuwahesabu katika aa'amali zao, na kuwalipa kulingana na matendo yao, kama ni kheri kwa kheri na kama ni shari kwa shari, malipo kwa waliyo ya fanya. { Naye ni Mwepesi kuliko wote wanao hisabu.} Aali-a'am : 62

#### "Mhasibu"

Aliyewazunguka na kuwajua kikweli kweli, anayejua kwa kina yaliyo ya dhahiri na yaliyojificha katika matendo ya waja wake.

Ewe Mola Mlezi ewe Utoshae, twakuomba ututosheleze katika yale ambayo yanatusumbua,na utuonyeshe njia ya uongofu,na utuzidishie kheri ewe Allah Mkarimu. {Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa Mhasibu.} (An-nisaa : 6)

Hakika yeye ni Allah Mhasibu Anayetosha.

## Allah yuko Wazi

Hakika Allah yuko Wazi

{ Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Haki Iliyo Wazi.} (Al-nnur : 25)

Ewe uliye Wazi jambo lako lililotukuka, tuwekee wazi njia ya haki,na utukinge na kuchanganyikiwa na njia za batili ewe Mola Mlezi.

Allah ndiye Mwenyekubainisha haki na haki zote, ndipo zidhihirike shaka zote.

Allah yuko Wazi katika jambo la upweke wake, na kwamba yeye hana mshirika yeyote katu.

#### "Aliye Wazi"

Hafichiki kwa waja wake kwa alama alizoziweka za kiakili na za kisheria na za kihisia na zakimaana zinazo-onesha uwepo wake Allah, zinazoonesha ufalme wake pia.

#### "Anayetosha"

Anawatoshelezea waja wake kwa yote wanayohitaji na kumlilia yeye, anawatoshelezea kutosheleza maalumu waja wake walio mwamini na kumtegemea na kuomba kwake haja zake za kidunia na za kiakhera.



**“Aliye Wazi”**

Aliye wabainishia waja wake njia ya sawa ya kweli, kwa kuteremsha Mitume(a.s) pamoja na vitabu vilivyo wazi kabisa. {Bila shaka imekujieni kutoka kwa Mwenyezi Mungu nuru na Kitabu kinacho bainisha.}(Al-maidah : 15)

Allah aliye bainisha njia ya furaha kwa waja wake na akaimbatanisha na kumtii yeye na kumpwekesha.

**Hakika yeye ni Allah Aliye Wazi**

**“Mwenye uwezo wajuu”**

Aliye na uweza uliokamilika, kwa uwezo wake aliumba viumbe, na kwa uweza kwake alivipanga, na kwa uwezo wake alivieka sawa na madhubuti, kwa uwezo wake anauhisha na kufisha, na kufufuwa waja kwa ajili ya malipo, amlipe mwema kwa wema wake na mkosa kwa makosa yake, ambae akitaka kitu anakiambia kiwe na kinakuwa, na kwa uwezo wake Allah Mtukufu anageuza nyoyo, na kuziendesha vile atakavyo.

**Allah Mwenye uweza Muweza.**

Hakika Allah ni Mwenye uweza { Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye uweza juu ya kila kitu.} (Al-baqarah : 284)

{Katika makalio ya haki kwa Mfalme Mwenye uweza (Al-qamar : 55)

{Sema: Yeye ndiye Muweza} (Al-ana'am : 65)

**“Mwenye uwezo”**

Mwenye nguvu, Madhubuti. Mwenye uweza wa kufanya ayatakayo.

**“Muweza”**

Uweza wa kamili , amehisha na kufisha akaumba viumbe akavipanga madhubuti.

**“Mwenye uweza wa juu”**

Atafufuwa watu na awalipe kwa uweza wake, anazipindua nyoyo vile atakavyo.

“Muweza”

Uweza uliokamilika haupatwi na upungufu hata kidogo.

“Muweza”

Mwenye kupanga waja wake kwa yale ayatakayo vile atakavyo, na huu ni katika ukamilifu wa uwezo wake .

Hakika Allah ni Muweza Mwenye uweza.

## Allah ni Mrithi

Hakika yeye ni Allah mrithi

{ Na Sisi ndio tunao huisha na tunao fisha. Na Sisi ndio Warithi.} (Al-hijri :23)

“ Mrithi”

Ambaye atarithi ardhi na vilivyomo, hakutabaki yeyote ila yeye Aliyetukuka ,

“ Mrithi”

Atakaye baki baada ya waja wake; kwa ukamilifu wa ufalme wake, kwa ufalme wake watarudi wafalme wote, anahofisha mwenye kudhulumu na kupita mipaka na kufanya ujeuri kwamba marudio ni kwake Allah kwasababu yeye ni Mrithi baada ya kufa viumbe vyote.

“ Mrithi”

Anawahimiza waja wake kutoa katika njia zake Mwenyezi Mungu Mtukufu,mali itaisha na umri utakwenda, na marejeo ni kwake Allah Mrithi.

“ Mrithi”

Anawahadharisha waja wake na kuacha kumshukuru, kwasababu asili ya neema ni kwake na marejeo yake ni kwake pia.

“ Mrithi”

Anarithi ardhi na vilivyomo , kwasababu kila mwenye kubakia baada ya kuondoka mwengine ni mrithi. { Na Sisi ndio tumekuwa warithi wao.} (Al-qasasi : 58)

Hakika yeye ni Allah Mrithi



## Allah Mwenye kusikia Mwenye kuona.

Hakika yeye Allah ni Mwenye kusikia Mwenye kuona.

Ewe Mwenye kusikia! Sikiza dua zetu na utuitikie maombi yetu; kwasababu wewe unaona matendo yetu na mapungufu yetu na haja zetu kwako.

“Allah Mwenye kusikia”

Anasikia sauti zote zilizo dhaifu na zilizo na nguvu, haimshughulishi sauti mpaka impite sauti nyengine, wala mwenye kuomba kwa mwengine.

“Allah Mwenye kuona”

Anaona kila kitu hata kama kitakuwa kidogo vipi au kikubwa vipi au kijifiche katika usiku au mchana.

“Mwenye kusikia”

Anasikia maneno hata kama lugha zitahitlafiana na kutafautiana maombi pia.

“Mwenye kuona”

Mwenye kumuona sisimizi mweusi katika usiku wa giza juu ya jabali jeusi, anaona yaliyoko chini ya ardhi ya saba, kama vile anavyoona juu ya mbingu ya saba.

“Mwenye kusikia Mwenye kuona”

Hakifichiki kitu kwake, wala hakipotei kidogo wala kikubwa.

Hakika yeye Allah ni Mwenye kusikia Mwenye kuona

## Allah Mwenye shukrani

Hakika Allah ni Mwingi wa shukrani Mwenye shukrani

Hakika Allah ni Mwingi wa shukrani {bila ya shaka Mwenyezi Mungu ni Mwenye shukrani na Mjuzi.} (Al-baqarah : 158) “Hakika Mola wetu Mlezi bila ya shaka ni Mwenye kusamehe, Mwenye shukrani” Faatri : 34

Yeye ni Allah Mtukufu Mwenye kushukuru matendo machache, na anasamehe makosa, na anawaongezea watu wema vitendo vyao bila ya hesabu.

“Mwenye kusikia Mwenye kuona”  
Anasikia maneno yako, basi jihesabu nafsi yako, na anasikia maombi yako basi mlimlie Mola wako, na anaona vitendo vyako hakuna kitu kinachofichika, basi fanya wema kwani Allah anawapenda watu wema.






**“ Allah Mwingi wa shukrani”**

Anampa mwenye kumshukuru, na anamfadhilisha mwenye kumuomba , na anamtaja mwenye kumtaja, mwenye kumshukuru atapata ziada, na kafiri atakuwa na hasara. { Mkishukuru nitakuzidishieni; na mkikufuru, basi adhabu yangu ni kali.} (Ibrahim : 7)

**Hakika Allah ni Mwingi wa shukrani Mwenye shukrani**



## Mwenye kusifika na kila sifa njema.

Hakika Allah ni Mwenye sifa njema

Mwenye sifa njema katika dhati yake, Mwenye sifa njema Katika vitendo vyake, Mwenye sifa njema katika maneno yake, Mwenye sifa njema katika tabia zake, hakuna Mwenye sifa njema katika ulimwengu huu isipokuwa Allah Mtukufu; Sifa zote njema sifa za kukamilika zote ni zake Allah.

Mwenye kusifika na sifa njema

Mwenye sifa njema katika dhati yake, na majina yake, na sifa zake, na vitendo vyake, ana majina yale mazuri mazuri na sifa zile zilizokamilika, na vitendo vilivyo vyema na vilivyokamilika, kwasababu vitendo vyake Allah vyote vinazunguka baina ya ubora na uadilifu.

Sifa njema zote ni zako peke yako kwa kututeremshia kitabu chako na ukatufahamisha utukufu wako na ukatumia Mtume wako Muhammad (s.a.w)

Hakika Allah ni Mwenye sifa njema.



## Allah Mkubwa Mwenye utukufu

Hakika Allah ni Mkubwa Mwenye utukufu na utakatifu

Hakika yeye ni Allah Mwenye kusifika na sifa za utukufu na ukubwa, ambaye ndiye Mkubwa kuliko chochote, na Mtukufu kuliko chochote, na Mtakatifu kuliko chochote,

Anatukuzwa na kuheshimiwa katika nyoyo za vipenzi vyake na wandani wake, zimejaa nyoyo zao utukufu wake na utakatifu wake, na kumnyenyekea yeye na kudhalilisha nafsi zao mbele ya ukubwa wa Allah.



Umetakasika Allah uliye Mkubwa ukubwa ulioje huu!! { Basi litakase jina la Mola wako Mlezi aliye Mkubwa.} (Al-waqiah : 96)

Hatuwezi kukusifu na kukutukuza kwa utukufu wako Ewe Mkubwa Ewe Mtukufu Ewe Mkarimu

Mkubwa katika dhati yake utukufu ni wake, ukubwa katika majina yake na sifa zake. { Hapana kitu kama mfano wake} (Ash'shuraa : 11)

Yeye ndiye Mwenye utukufu na ukubwa , mwenye kugombana naye katika haya, Allah atamvunja; kama alivyo sema Allah katika hadiith qudsi; Ukubwa ni nguo yangu ya juu na utukufu ni nguo yangu ya chini Mwenye kuichukua moja katika hizi nguo nitamuingiza motoni' (Imepokewa na Muslim)

Hakika Allah Mwenye utukufu Mwenye Ukubwa na Utakatifu

## Allah Aliye juu ya walio juu Aliyetukuka

Hakika Allah ni Aliye juu ya waliojuu Aliye tukuka

**"Aliye juu ya waliojuu Aliye tukuka"**

Yuko na utukufu kamili katika sura zote, utukufu wa dhati, utukufu wa uwezo wake na sifa zake utukufu wa kuteza nguvu kwake. { Na Yeye ndiye aliye juu, na ndiye Mkuu.} (Al-baqarah : 255)

Amestawi juu ya arshi, na kwa sifa zote tukufu, na ukubwa na heshima zote na uzuri alisifika, na kwake ndio zimekamiliika.

**“Aliye juu ya Walio juu”**

Ametakasika na kila sifa ambayo hailingani naye, na kila upungufu wenye kutokea, imetakasika dhati yake na sifa zake na uwezo wake, ni Allah aliyetukuka.

**Hakika Allah ni Aliye juu ya walio juu Aliyetukuka**

## **Allah Mwenye kuzuia au kunyima Mwenye kutoa.**

Hakika Allah ni Mwenye kuzuia au kunyima Mwenye kutoa.

**“Mwenye kuzuia au kunyima”**

Anawazuilia watu riziki ili awapime na kuwaonja, na anawanyima wengine kwa kuwaadhibu, na anawahifadhia wengine ili awainue daraja.

**“Allah Mwenye kutoa.”**



Anakunjua na kutoa riziki, na anatoa maarifa katika kila moyo, yote haya kulingana na hekima yake na rehema zake na ukarimu wake Allah Mtukufu.

Hakika Allah ni Mwenye kuzuia au kunyima, Mwenye kutoa.

## Allah Mwenye kutoa Mwenye kuzuia

Hakika Allah ni Mwenye kutoa Mwenye kuzuia

Allah Mwenye kutoa, Mwenye kuzuia

Hakuna Mwenye kuzuia Aliyempa Allah, wala hakuna wakumpa aliyenyimwa na Allah, maslahi yote na manufaa yote yanaombwa kwake, na yake yanapendwa, nayeye ndiye anampatia amtakaye, na anamnyima amtakaye kwa hekima yake na rehema yake.

Ewe Allah Mwenye kutoa twakuomba utupe rehema zako, utupe unavyotoa, na utuzuilie mabaya yote Ewe Mwenye kuzuia, na uizuie shari na maovu yasisibu, Ewe Mwenye kuzuia.

Hakika Allah Mwenye kutoa Mwenye kuzuia

Sifa zote njema ni za Allah, kama alivyojisifu Mwenyewe, kuliko wanavyomsifu viumbe vyake.

Imamu Ash-shafi